Shushani ngomeni ni sehemu gani kwasasa?

Mji wa shushani/Susa kwasasa upo eneo linaloitwa Shush katika nchi ya Iran.

kabla wamedi na waajemi kuiangusha Babaeli, Shushani ulikuwa ni mji mkuu wa Elamu, ambao tunaona Danieli akiuzungumzia katika.

> *Danieli 8:1 “Katika mwaka wa tatu wa kumiliki kwake mfalme Belshaza maono yalinitokea mimi, naam, mimi Danieli, baada ya hayo yaliyonitokea hapo kwanza.*
>
> *2 Nami naliona katika maono; ilitukia, nilipoona, nalikuwako huko Shushani ngomeni, katika wilaya ya Elamu; nikaona katika maono, nami nalikuwa karibu na mto Ulai”.*

Lakini baada ya wamedi na waajemi kuuchukua ufalme, mji huu ulikuja kugeuzwa kuwa mji wa kifalme wa wafalme wa Uajemi na Umedi.

Katika biblia tunaona Esta aliishi sehemu kubwa ya umalkia wake katika mji huu wa kifalme Shushani.

> *Esta 1:1 Zamani za Ahasuero; naye huyu Ahasuero alimiliki toka Bara Hindi mpaka Kushi, juu ya majimbo mia na ishirini na saba;*
>
> *2 siku zile mfalme Ahasuero alipoketi katika kiti cha enzi cha ufalme wake, huko Shushani ngomeni;*

Unaweza kusoma pia, (Esta 2:3,5,8 Esta 3:15, Esta 4:8,16, Esta 8:14, Esta 9:6,11,12,13.)

Vilevile Nehemia naye alipokuwa mnyweshaji wa mfalme wa kiajemi alikuwa katika mji huu, huu wa Shushani..

> *Nehemia 1:1 “Habari za Nehemia, mwana wa Hakalia. Ikawa katika mwezi wa Kisleu, mwaka wa ishirini, nilipokuwapo Shushani ngomeni,*
>
> *2 Hanani, mmoja wa ndugu zangu, akanijia, yeye na watu*

> *wengine waliotoka Yuda; nami nikawauliza habari za Wayahudi waliopona, hao watu wa uhamisho waliosalia; na habari za Yerusalemu”.*

Ikiwa utapenda tuwe tunakutumia masomo ya biblia ya mara kwa mara kwa njia ya whatsapp au email yako, basi tutumie ujumbe kwa kupitia namba hii: +255 789001312

Mada Nyinginezo:

> *MTO YORDANI UKO NCHI GANI KWA SASA?*

> *Mto Frati upo nchi gani, Umuhimu wake katika biblia ni upi?*

> *Israeli ipo bara gani?*

> *UNYAKUO.*

> *MAPIGO YA VITASA SABA, NA SIKU YA BWANA.*

Rudi Nyumbani:

Share on:
WhatsApp